

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA



HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA NJOMBE

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe anapenda kuwatangazia watazania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe kuomba nafasi za kazi za mkataba zilizotajwa hapo chini kuwasilisha maombi yao.

**1. AFISA MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA LA II (NURSE II) NAFASI 05**

**a) Sifa za kuajiriwa:**

Kuajiriwa wenye Aatahahada katika fani ya Uguzi kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali na ambao wamesajiliwa na baraza (Tanzania Nursing and Midwifery Council)

**b) Kazi na Majukumu:**

- i. Kutoa huduma za Uguzi
- ii. Kukusanya takwimu muhimu za Afya
- iii. Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
- iv. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- v. Kutoa huduma za kinga na uzazi
- vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**2. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II (NAFASI 02)**

**a) Sifa za kuajiriwa**

Kuajiriwa mwenye Stashahada ya utunzaji kumbukumbu kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali.

**b) Kazi na Majukumu**

- i. Kupokea nyaraka zilitoka nje na ndani ya taasisi na kuziweka katika Mafaili
- ii. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/mafaili yanayohitajika na watumiaji
- iii. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu katika makundi kulingana na somo husika kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
- iv. Kuweka/kupanga kumbukumbu katika reki/katika masijala/vyumba vya uhifadhi kumbukumbu.
- v. Kuweka kumbukumbu ya (barua,nyaraka n.k) katika mafaili
- vi. Kutunza na kudhibiti upotevu wa nyaraka na kuhakikisha nyaraka hizo hazitolewi kwa asiyehusika nazo.

**3. MHUDUMU WA AFYA (JENGO LA KICHOMEA TAKA) Nafasi 01**

**a) Sifa za kuajiriwa**

- i. Awe Mtanzania mwenye umri usiozidi miaka 45
- ii. Awe na elimu ya Sekondari

**b) Kazi na Majukumu**


- i. Kuteketeza taka zote zinazozalishwa Hospitalini
- ii. Kutunza na kukagua mtambo wa kuteketeza taka kabla na baada ya kuteketeza taka
- iii. Kutunza jengo la kichomea taka
- iv. Kuandaa taarifa za wiki na mwezi za taka zilizoteketezwa
- v. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu,uzoefu na ujuzi wake.

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE**

- i) Awe na umri usiozidi miaka 35 na mwenye afya njema
- ii) Waombaji waambatishe wasifu (Curriculum Vitae) yenye anwani sahihi, namba za simu sahihi, pamoja na majina mawili ya wadhamini (watumishi wa serikali) na namba zao za simu zinazopatikana
- iii) Barua za Wadhamini wawili zikiwa na anwani zao sahihi na namba za simu
- iv) Awe na vyeti husika vya Taaluma. Testimonial "provisional results" statement of results, hati ya matokeo ya kidato cha nne **HAVIKUBALIKI**
- v) Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na TCU au NECTA
- vi) Waombaji waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo vilivyothibitishwa;
  - a) Cheti cha kuzaliwa
  - b) Cheti cha kuhitimu elimu ya kidato cha nne
  - c) Cheti cha kuhitimu elimu ya kidato cha sita
  - d) Vyeti vya taaluma
  - e) Leseni kutoka mabaraza husika

f) Cheti cha kompyuta  
vii) Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **14 Aprili, 2026**  
Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Posta au moja kwa:-

**MGANGA MFAWIDHI,  
HOSPITALI YA RUFEE YA MKOA WA NJOMBE,  
S. L. P 1044,  
NJOMBE**

  
*Imetolewa na Ofisi ya Habari na Uhusiano  
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe  
01 Aprili, 2026*